# RUVUMA INAVYOJIVUNIA MIAKA MITATU YA RAIS

# SAMIA SULUHU HASSAN












**JARIDA HILI LIMEANDALIWA NA SEKRETARIETI YA MKOA WA RUVUMA KUPITIA KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI**

rs ruvuma

www.ruvuma.go.tz

# KARIBU MKOA WA RUVUMA



Haki zote zimehifadhiwa.Hairuhusiwi kuiga, kunakili, kutafsiri, kupigachapa, kutoa nakala kivuli au kutoa baadhi ya maandishi ya Jarida hili kwa namna yoyote ile bila idhini ya Mwandishi kwa maandishi.

Jarida limehaririwa na Albano Midelo wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini (GCU) Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma

## YALIYOMO

1.Rais Samia anavyowatua ndoo kichwani wananchi wa Ruvuma

2.Bilioni 7.2 zilivyojenga shule mpya za msingi Ruvuma

3.Miaka mitatu ya Rais Samia ilivyoboresha sekta ya afya Ruvuma

4.Rais Samia atoa vifaa tiba vya milioni 760 Ruvuma

5.Madini na kilimo vilivyoupaisha Mkoa wa Ruvuma

6.Wanawake Ruvuma wakopeshwa bilioni tatu za Samia

7.Bilioni 2.24 zinavyotekeleza miradi ya maji Songea

8.TANROADS Ruvuma inavyojivunia miaka mitatu ya Rais Samia

9.Mradi wa maji Ngumbo kumaliza kero ya maji

10.Serikali yatoa bilioni 66 kujenga miradi ya maji 36 Ruvuma

11.Wananchi Ruvuma wamshukuru Rais Samia kwa bandari ya Ndumbi

12.Rais Samia aleta tabasamu kwa wanafunzi wa kike Ruvuma

13.Miaka mitatu ya Rais Samia,ujenzi wa bandari ya kisasa Mbambabay waanza

14.Kero ya maji Songea kubakia historia

15.Ruvuma kupanda miti hekta 100,000

16.Bandari ya Ndumbi kuunganishwa na lami

17.Rais Samia atoa mbolea ya ruzuku tani 93,000 Ruvuma

18.RC Ruvuma anavyotekeleza maagizo ya Rais ya kujeenga mahusiano na nchi jirani

19.Msumbiji kuunganishwa na uwanja wa ndege Songea

20.TARURA Ruvuma yatengewa bilioni 22.5 kuboresha miundombinu

**TAHARIRI**

Wapendwa wasomaji wetu ninayoheshima kubwa kuwaalika katika Kitengo cha Mawasiliano Serikalini (GCU) ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma kusoma habari na makala mbalimbali ambazo zinakuwa zinachapishwa na jarida hili.

Jarida hili ni sehemu ya utekelezaji wa mwongozo uliotolewa na Ofisi ya Rais TAMISEMI kupitia kitengo cha Mawasiliano Serikali kuhakikisha kila mwezi GCU Mkoa na Halmashauri zake zinachapisha jarida ili kutangaza shughuli mbalimbali zinazofanywa na serikali ikiwemo kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo, mahusiano na kutangaza fursa za utalii na uwekezaji zilizopo katika Mkoa wa Ruvuma na namna viongozi wanavyosikiliza kero za wananchi na kuzitafutia ufumbuzi.

Furahia kusoma





## RAIS SAMIA ANAVYOWATUA NDOO KICHWANI WANANCHI WA RUVUMA



***Kamati ya Kudumu ya Maji na Mazingira ya Bunge ilipotembelea kukagua mradi wa maji katika Kata ya Tingi wilayani Nyasa mkoani Ruvuma***

WANANCHI wa Mkoa wa Ruvuma wanaendelea kunufaika na uongozi wa serikali ya Awamu ya Sita ambapo katika kipindi cha mwaka 2022/2023 serikali ilitenga bajeti ya zaidi ya shilingi bilioni 28.7 kutekeleza miradi ya maji mkoani Ruvuma.

Meneja wa Wakala wa Maji Mijini na Vijijini (RUWASA) Mkoa wa Ruvuma Mhandisi Rebman Ganshonga anasema hadi sasa serikali imeleta zaidi ya shilingi bilioni 19 kutekeleza miradi hiyo katika wilaya za Songea, Mbinga, Nyasa ,Namtumbo na Tunduru.

Anasema katika kipindi cha mwaka 2023/2024 serikali imetenga zaidi ya shilingi bilioni 26.2 kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maji mkoani Ruvuma.

Anaitaja baadhi ya miradi iliyoidhinishiwa fedha wilayani Mbinga kuwa ni mradi wa maji Linda milioni 450,mradi wa maji Tukuzi milioni 450,mradi wa maji Mtama milioni 400,mradi wa maji Kipololo milioni 400,mradi wa maji Kigonsera milioni 300 na mradi wa maji Ngima milioni 253.

Katika Wilaya ya Songea miradi iliyoidhinishiwa fedha anaitaja kuwa ni mradi wa maji Lwangeni milioni 618,mradi wa maji Lipaya bilioni 1.9,mradi wa maji Lipokela milioni 734.74,mradi wa maji Kizuka milioni 730.4,mradi wa maji Mtyangimbole bilioni 5.56 na mradi wa maji Ndelenyuma bilioni 1.6.

Meneja huyo wa maji Mkoa wa Ruvuma anaitaja baadhi ya miradi ya maji katika Wilaya ya Nyasa kuwa ni ukarabati wa mradi wa maji Ng'ombo shilingi milioni 130,ukarabati wa mradi wa maji Lunyele milioni 280,mradi wa maji Mbuyula-Ndengele shilingi milioni 649.86 na mradi wa maji Mitomoni milioni 944.

Mhandisi Ganshonga anaitaja miradi ya maji iliyoidhinishiwa fedha katika kipindi cha mwaka 2023/2024 wilayani Namtumbo kuwa ni mradi wa maji Naikesi milioni 179.5,mradi wa maji Likusanguse milioni 300,mradi wa maji Mchomoro milioni 320.14 na mradi wa maji Msisima milioni 168.

Miradi ya maji katika wilaya ya Tunduru anaitaja kuwa ni mradi wa maji Namwinyu milioni 535,mradi wa maji Hulia milioni 300,mradi wa maji Tuwemacho milioni 150,mradi wa maji Msinji milioni 200,Mradi wa maji Msechela milioni 200,mradi wa maji Nakapanya milioni 150 na mradi wa maji Masonya milioni 94.95.

"Utekelezaji wa miradi hiyo umeongeza huduma za upatikanaji wa maji kutoka asilimia 58.4 mwaka 2018 hadi kufikia asilimia 70 mwaka 2023,kuongeza huduma ya maji kutoka watu 891,616 mwaka 2018 hadi kufikia watu 1,035,325 mwaka 2023'',anasema Ganshonga.

Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Kanali Ahmed Abbas Ahmed anasema asilimia 70 ya watu wanaoishi vijijini mkoani Ruvuma ambao ni 1,294,156 kulingana na sensa ya watu ya mwaka 2022 wanapata huduma ya maji safi na salama ambapo lengo la Mkoa ni kufikia asilimia 85 kupata maji safi na salama kwa wakazi wa vijijini ifikapo mwaka 2025.

Kanali Abbas anabainisha kuwa Rais Dkt.Samia ameongeza idadi ya vijiji vyenye huduma ya maji kufikia 366 kati ya vijiji 533 vilivyopo Mkoani Ruvuma.

Anasisitiza kuwa Rais Dkt.Samia Suluhu Hassan amedhamiria kuwatua ndoo kichwani wananchi wa Mkoa wa Ruvuma na kwamba hadi kufikia Juni 30,2023 Mkoa wa Ruvuma ulikuwa unatekeleza jumla ya miradi 33 ya maji yenye thamani ya zaidi ya shilingi bilioni zaidi ya bilioni 55.

Naye Mhandisi wa Maji Wilaya ya Songea Mhandisi Mathias Charles anampongeza Rais Dkt Samia Suluhu Hassan kwa kutoa shilingi bilioni 11.2 katika Wilaya hiyo ili kutekeleza miradi sita ya maji katika kipindi cha mwaka 2023/2024.

Stella Mhagama Mkazi wa Kijiji cha Lipaya wilayani Songea anamshukuru Rais Dkt.Samia Suluhu Hassan kwa kutoa fedha za kutekeleza mradi wa maji ambapo anasema kwa miaka mingi wanawake na Watoto wamekuwa wanapata kero ya kusafiri umbali mrefu kufuata maji mtoni na kubeba kichwani.

Diwani wa Kata ya Mpitimbi wilayani Songea Mheshimiwa Issa Kindamba anampongeza Rais Dkt.Samia kwa kutoa fedha nyingi za kutekeleza mradi wa maji Lipaya ambao anasema unakwenda kupunguza umbali wa wananchi kutembea kufuata maji na kupunguza magonjwa yanayosambazwa na maji yasiyo salama.

Romanus Ndunguru Mkazi wa Kijiji cha Utili wilayani Mbinga anaishukuru serikali ya Awamu ya Sita kwa kuwajengea mradi wa maji Utiri kwa gharama ya shilingi milioni 428 ambao umekamilika kwa asilimia 99 na unakwenda kuhudumia watu 3,626.

Anania Nkomola Mkazi wa Kijiji ch Hinga wilayani Nyasa kwa niaba ya wananchi wenzake anamshukuru Rais Dkt.Samia Suluhu Hassan kwa kuwajengea mradi mkubwa wa maji Ngumbo wenye thamani ya shilingi bilioni 2.5 ambao tayari wananchi wameanza kunufaika nao.

Wananchi wa Kata ya Liuli wanamshukuru Rais Dkt.Samia Suluhu Hassan kwa kutekeleza mradi wa maji katika Kijiji cha Hongi Kata ya Liuli wilayani Nyasa ambao umegharimu shilingi bilioni 4.7 ambapo hadi sasa mradi umeanza kuwahudumia wananchi.

Mrad mwingine mkubwa wa maji wilayani Nyasa ni ule ambao unatekelezwa katika kijiji cha Mwerampya kata ya Lituhi unaogharimu shilingi bilioni 6.5 ambapo tayari baadhi ya vijiji vimeanza kunufaika na mradi huo.

Nao wakazi wa Misechela wilayani Tunduru akiwemo Amina Mohamed na Mariam Hussein wanaishukuru serikali kwa kuanza kutekeleza mradi mkubwa wa maji ya bomba wenye thamani ya shilingi bilioni tatu ambapo wananchi hivi sasa wanapata huduma ya maji katika visima vinavyotumia pampu za mkono.

Hakuna ubishi wananchi wa Mkoa wa Ruvuma na Taifa kwa ujumla moja ya vitu ambavyo watamkumbuka Rais Dkt.Samia Suluhu Hassan ni namna anavyoshughulikia kwa ufanisi wa hali ya juu changamoto ya upatikanaji wa maji safi na salama kwa wananchi wa vijijini na mijini.



*Tanki la mradi wa maji Malungu Kata ya Tingi wilayani Nyasa mradi ambao serikali imetoa zaidi ya shilingi bilioni moja ili kuhakikisha wananchi wanapata maji safi*

## RAIS SAMIA ATOA BILIONI 7.2 KUJENGA SHULE MPYA 12 ZA MSINGI RUVUMA



***Hawa ni wanafunzi wanaosoma katika shule mpya ya msingi Nahange kata ya Namtumbo iliyojengwa kupitia mradi wa BOOST***

RAIS wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt.Samia Suluhu Hassan ametoa shilingi bilioni 7.2 kupitia mradi wa BOOST kujenga shule 12 mpya za msingi na miundombinu mbalimbali katika shule 44 mkoani Ruvuma.

Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Kanali Ahmed Abbas Ahmed amesema fedha hizo zimetolewa katika mwaka wa fedha za 2022/2023 na kwamba kati ya fedha hizo zaidi ya shilingi bilioni 4.34 zimetumika kujenga shule mpya.

Amebainisha kuwa ujenzi wa shule hizo mpya umehusisha ujenzi wa madarasa ya msingi 98,madarasa ya elimu ya awali ya mfano 24,matundu ya vyoo ya elimu ya msingi 136 na matundu ya vyoo ya elimu ya awali 72.

Miundombinu mingine katika shule hizo ameitaja kuwa ni matundu ya vyoo vya walimu 24,vichomea taka 12 na majengo ya utawala 12.

Kwa mujibu wa Mkuu wa Mkoa zaidi ya shilingi bilioni 2.9 zimetumika kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu mbalimbali ambayo inahusisha madarasa ya msingi 87,matundu ya vyoo ya msingi 114,madarasa ya elimu ya awali 16,matundu ya vyoo vya awali 48 na nyumba za walimu mbili.

Kwa upande wake Afisa Elimu Mkoa wa Ruvuma Mwl.Edith Mpinzile amesema Mkoa umepokea shilingi milioni 264 kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa vituo vya walimu 12 katika Halmashauri zote nane za Mkoa.

“Mkoa pia umepokea shilingi bilioni 1.56 kupitia mradi wa SWASH kwa ajili ya ujenzi wa matundu ya vyoo 607 katika shule za msingi 47 na ujenzi upo katika hatua mbalimbali”,alisema Mpinzile.

Akizungumzia elimu maalum,elimu ya watu wazima na elimu nje ya mfumo rasmi,Afisa Elimu huyo Mkoa amesema hadi kufikia Novemba 2022,Mkoa ulikuwa na vituo 109 katika shule za msingi vinavyotekeleza mpango wa Elimu ya msingi kwa Watoto walioikosa (MEMKWA).

Amesema Mkoa wa Ruvuma hivi sasa una vituo 302 katika shule za msingi na sekondari vyenye Watoto wenye mahitaji maalum.

Hata hivyo amesema idadi ya Wanafunzi wasiojua KKK kwa darasa la kwanza na la pili imeendelea kupungua kutoka wanafunzi 7,427 mwezi Juni 2023 hadi kufikia 6,188 mwezi Desemba 2023 ikiwa ni sawa na asilimia 16.6.

Ameitaja mikakati ya kuinua elimu na kuongeza taaluma kuwa ni kufanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa mtaala wa elimu katika ngazi za Halmashauri na shule,kuhimiza utoaji motisha kwa wanafunzi na walimu katika shule zinazofanya vizuri kwenye taaluma na kuhimiza wananchi utoaji chakula kwa wanafunzi wawapo shuleni.

Naye Mwalimu Mkuu shule mpya ya Msingi Nahange iliyojengwa kupitia mradi wa BOOST iliyopo Kata ya Suluti wilayani Namtumbo Mwl. Nahale Ponera amesema serikali imetoa shilingi milioni 331.6 kujenga shule hiyo ambayo imeanza tangu

Amesema shule hiyo ina jumla ya wanafunzi 529 wanaosoma katika vyumba tisa kuanzia awali hadi darasa la saba ambapo wanamshukuru Rais Dkt.Samia kwa kutoa fedha za kujenga shule hiyo inayovutia wanafunzi kutokana kuwa na miundombinu ya kisasa.

Shaban Nyahale ni Mwanafunzi shule mpya ya msingi Mzalendo iliyopo Kata ya Masuguru wilayani Namtumbo amesema anamshukuru Rais Samia kwa kuwajengea shule yenye mazingira rafiki kwa kusomea.

## MIAKA MITATU YA RAIS SAMIA ILIVYOBORESHA SEKTA YA AFYA



### Hospitali ya Rufaa Ruvuma ilivyopunguza adha ya wagonjwa kwenda Muhimbili

SERIKALI ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais Dkt.Samia Suluhu Hassan kupitia Wizara ya Afya imetenga zaidi ya shilingi bilioni 6.57 kutekeleza mradi wa hospitali ya Rufaa ya Mkoa,Songea.

Fedha hizo ni kwa ajili ya ujenzi wa majengo mapya,ukarabati wa vyumba vya kutolea huduma za afya na ununuzi wa vifaa tiba vya kisasa kwa ajili ya kutolea huduma bora za afya kwa wananchi wa Mkoa wa Ruvuma.

Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Kanali Ahmed Abbas Ahmed anasema katika mwaka wa fedha 2023/2024 Wizara ya Afya imetenga kiasi cha shilingi bilioni moja kwa ajili ya ukamilishaji wa ujenzi wa jengo wagonjwa wa nje (OPD).

“Kwa niaba ya wananchi wa Mkoa wa Ruvuma napenda kutoa pongezi za dhati Rais Dkt.Samia Suluhu Hassan kwa kutoa mabilioni ya fedha kutekeleza miradi ya afya hivyo kujali afya za watanzania wa Mkoa wa Ruvuma’’,anasema Kanali Thomas.

Akizungumzia utekelezaji wa mradi huo, Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa,Songea Dr. Magafu Majura anayataja majengo yaliyokamilika kwa asilimia 100 kuwa ni ujenzi wa nyumba ya daktari,ujenzi wa jengo la radiolojia kwa ajili ya CT Scan,Digital X Ray na ukarabati wa wodi ya wagonjwa wanaohitaji uangalizi wa karibu (ICU).

Dr.Majura anayataja majengo mengine ambayo yamekamilika kwa asilimia 100 kuwa ni ukarabati wa chumba cha tiba masafa (Telemedidicine), ununuzi wa vifaa kwa ajili ya majengo ya wagonjwa mahututi (ICU),jengo la dharura (EMD),maabara na radiolojia.

“Kutokana na ufinyu wa eneo la hospitali ya Rufaa ya Mkoa,Songea,Mkoa uliona umuhimu wa kuwa eneo jipya lenye ukubwa wa hekari 270 katika Kata ya Mwengemshindo Manispaa ya Songea,ambako kumeanzisha ujenzi wa hospitali mpya ya Rufaa ya Mkoa wa Ruvuma’’,anasema Dr.Majura.

Analitaja jengo muhimu ambalo wameanza nalo ni la wagonjwa wa nje (OPD) ambapo anasema mradi wa jengo hilo unagharimu zaidi ya shilingi bilioni 3.8 ambapo hadi sasa jengo limefikia asilimia 71.

Akizungumzia jengo la radiolojia,Mganga Mfawidhi huyo anasema katika jengo hilo ndani yake kuna mashine mbili za CT Scan na Digital Xray ambazo zinafanya kazi na kwamba vifaa hivyo vina thamani ya zaidi ya shilingi bilioni mbili.

Anasema huduma za CT Scan zilianza kutolewa Machi 2023 hali ambayo imepunguza adha kwa wananchi wa Mkoa wa Ruvuma na mikoa jirani ambao awali walikuwa wanapata huduma hiyo katika hospitali ya Kanda ya Mbeya na hospitali ya Taifa Muhimbili.

Akizungumzia utekelezaji wa miradi ya afya,Mganga Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Dr.Louis Chomboko anasema katika kipindi cha mwaka 2023/2024 serikali imetoa shilingi bilioni 1.8 kutekeleza miradi ya afya katika hospitali za Halmashauri za Madaba na Manispaa ya Songea.

Anabainisha kuwa hospitali ya Halmashauri ya Madaba imepewa shilingi milioni 800,Halmashauri ya Manispaa ya Songea imepewa milioni 800 na kwamba shilingi milioni 200 zimetolewa kwa ajili ya ujenzi wa zahanati za Ifinga, Likuyufusi,Litoromelo na Litindoasili.

Akizungumzia huduma za Afya ya uzazi na mtoto,Dr.Chomboko anavitaja vituo vinavyotoa huduma ya uzazi na mtoto vimefikia 348 kati ya vituo 419 sawa na asilimia 83 ya vituo vyote vinavyotoa huduma katika Mkoa.

Anabainisha kuwa vituo 325 sawa na asilimia 78 vinatoa huduma ya chanjo,kati ya vituo vya afya 50,vituo 17 sawa na asilimia 34 ya vituo vya afya vinatoa huduma kabambe za dharura za mama wajawazito na Watoto wachanga.

Kulingana na Mganga Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma,kiwango cha akinamama waliojifungua kituoni kimeongezeka kutoka asilimia 84 mwaka 2022 hadi asilimia 87 hadi kufikia Desemba 2023.

Anasema vifo vya Watoto chini ya mwaka mmoja kwa mwaka 2023 vimeendelea kupungua kutoka 232 mwaka 2022 hadi vifo 131 mwaka 2023.

Akizungumzia hali ya utoaji chanjo,Dr.Chombo anasema kwa mwaka 2023 chanjo ya kifua kikuu imetolewa kwa asilimia 166,chanjo ya polio asilimia 135,chanjo ya dondakoo,kukakamaa na kifaduro zimetolewa kwa asilimia 135.

Kwa mujibu wa Mganga Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma,chanjo ya kuzuia homa ya mapafu imetolewa kwa asilimia 135,chanjo ya kuzuia kuharisha asilimia 127,chanjo ya surua asilimia 152,chanjo ya pepopunda kwa wajawazito asilimia 106 na chanjo ya kuzuia saratani ya mlango wa kizazi kwa wasichana wenye umri wa miaka 14 ni asilimia 126.

Dr.Hussein Ngaila ni Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Wilaya ya Nyasa anasema serikali imetoa zaidi ya bilioni tatu kukamilisha ujenzi wa hospitali hiyo ambao umefanyika kwa awamu tatu.

Anasema katika awamu ya kwanza serikali ilitoa bilioni 1.5 kujenga majengo saba ambayo ni jengo la utawala, mionzi, famasia,maabara,wagonjwa wa nje na huduma za mama na mtoto.

Kulingana na Dr.Ngaila awamu ya pili ya ujenzi ilihusisha majengo matatu ambayo ni wodi ya wanawake,wodi ya wanaume na wodi ya Watoto ambapo jumla ya milioni 490 zilitumika.

Katika awamu ya tatu serikali imetoa shilingi milioni 800 kujenga majengo manne ambayo ni jengo la upasuaji,wodi mbili za upasuaji kwa wanawake na wanaume,jengo la kuhifadhia maiti na ujenzi wa jengo la huduma za dharura (EMD) ambalo limegharimu shilingi milioni 300.

Naye Mganga Mfawidhi wa hospitali ya Wilaya ya Tunduru Dr.Athumani Mkonoumo anasema serikali imetoa shilingi milioni 900 kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa hospitali hiyo kongwe nchini iliyojengwa mwaka 1930.

Anasema fedha hizo zimejenga jengo la wagonjwa wa nje OPD,maabara na ukarabati mkubwa wa jengo la upasuaji na kwamba serikali imetoa shilingi milioni 300 kwa ajili ya jengo la huduma za dharura EMD.

Anasema serikali pia imetoa vifaa tiba kwa ajili ya jengo la EMD na hospitali ambavyo anavitaja kuwa ni mashine ya xray,ultrasound ya kisasa,mashine za kusaidia kupumua na mashine mbalimbali za maabara.

Dr.Chacha Wambura ni Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Madaba anasema serikali ya Awamu ya Sita pia imetoa zaidi ya shilingi bilioni tatu kutekeleza mradi wa ujenzi wa hospitali ya Halmashauri ya Madaba mradi ambao umekamilika na umeanza kuwahudumia wananchi.

Mkoa wa Ruvuma una vituo 419 vinavyotoa huduma za afya,kati ya vituo hivyo hospitali zipo 17,vituo vya afya 50 na zahanati 352.

## RAIS SAMIA ATOA VIFAA TIBA VYA MILIONI 760 RUVUMA



***Kulia ni aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma akimkabidhi vifaa tiba Mwakilishi wa wabunge wa Mkoa wa Ruvuma Mheshimiwa Benaya Kapinga***

RAIS wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt.Samia Suluhu Hassan ametoa vifaa tiba vyenye thamani ya shilingi milioni 760 katika vituo 18 vya kutolea huduma za afya mkoani Ruvuma.

Hafla ya makabidhiano ya vifaa tiba hivyo kutoka Bohari Kuu ya Dawa (MSD) imefanyika kwenye viwanja vya Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma mjini Songea.

Akizungumza kwenye hafla hiyo mgeni rasmi aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Kanali Laban Thomas amesema vifaa tiba hivyo vitasambazwa katika vituo 18 vya kutolea huduma za afya kwa awamu mbili ambapo katika awamu ya kwanza itahusisha usambazaji wa vitanda vya hospitali,magodoro na mashuka.

Amesema vifaa hivyo vinasambazwa na MSD Kanda ya Iringa na Mtwara kuanzia Machi 6,2024 kwenye vituo vilivyopo katika majimbo ya uchaguzi na Halmashauri za Mkoa wa Ruvuma.

“Ni Dhahiri kabisa ujio wa vifaa tiba hivi utasaidia kuboresha huduma za afya ,tunaishukuru Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais Dkt.Samia Suluhu Hassan kwa maboresho makubwa katika sekta ya afya’’,alisema RC Thomas.

Kwa upande wake Mganga Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Dr.Louis Chomboko amesema vifaa tiba hivyo vimeletwa na serikali kwa mwamvuli wa majimbo tisa ya uchaguzi mkoani Ruvuma ili kuimarisha afya za wananchi hatimaye waweze kushiriki vema katika shughuli za maendeleo.

Hata hivyo amesema kutolewa kwa vifaa hivyo ni sehemu tu ya vifaa tiba kwa sababu serikali bado inaendelea kuleta dawa na vifaa tiba kupitia MSD ambapo katika kipindi cha kuanzia Julai 2023 hadi sasa Mkoa wa Ruvuma umepokea shilingi bilioni 2.9 kutoka serikali kuu kwa ajili ya ununuzi wa vifaa tiba.

Naye Mbunge wa Jimbo la Mbinga Vijijini Benaya Kapinga akizungumza kwa niaba ya wabunge wa Mkoa wa Ruvuma, amemshukuru Rais Dkt.Samia Suluhu Hassan kwa kuleta vifaa hivyo ambavyo amesema vimeleta faraja kwa wananchi wa Mkoa wa Ruvuma.

Mwakilishi wa Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Ruvuma Komred John Haule amesema wataendelea kumpongeza Rais Dkt.Samia Suluhu Hassan kwa kuwa anafanya vitu vinavyoonekana kwa wananchi.

Amewaasa watumishi wa afya mkoani Ruvuma kuhakikisha kuwa vifaa hivyo wanavitunza na vinatumika kwa malengo yaliyokusudiwa

Ofisi ya Rais TAMISEMI imenunua vifaa tiba mbalimbali kwa ajili ya vituo vya kutolea huduma za afya vilivyopo katika majimbo 214 nchini yakiwemo majimbo tisa ya Mkoa wa Ruvuma

## MADINI NA KILIMO VILIVYOUPAISHA MKOA WA RUVUMA



***Waziri Mkuu Mheshimiwa Kassim Majaliwa alipotembelea mgodi wa kuzalisha makaa ya mawe wa JITEGEMEE wilayani Mbinga***

PATO la Taifa katika Mkoa wa Ruvuma limeongezeka kutoka shilingi bilioni 2.37 mwaka 2012 hadi kufikia bilioni 6.39 mwaka 2022.

Kwa mujibu wa takwimu kutoka Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) uchumi wa Kanda ya kusini Mashariki ukiwemo Mkoa wa Ruvuma unaendelea kuimarika.

Kulingana na NBS Pato la Taifa (GDP) katika kanda hiyo limekuwa linaongezeka mwaka hadi mwaka na kufanya kanda hiyo kuchangia wastani wa asilimia 10.5 ya Pato la Taifa katika Mkoa wa Ruvuma.

Kwa mujibu wa NBS ongezeko hilo limechangiwa Zaidi na uzalishaji katika shughuli za kilimo na madini.

Katika mwaka 2022,Mkoa wa Ruvuma ulichangia asilimia 3.8 ya Pato la Taifa na kuwa juu ya mikoa mingine ya Kanda ya Kusini Mashariki iliyochangia kati ya asilimia 2.0 na asilimia 2.8 .

Katika kipindi cha miaka kumi iliyopita wastani wa pato kwa mtu GDP katika wa Ruvuma limeongezeka kwa Zaidi ya maradufu na kuwa juu ya wastani wa pato kwa mtu kitaifa.

Hata hivyo kulingana na NBS wastani wa pato kwa mtu kwa mwaka kwa Mkoa wa Ruvuma uliongezeka kutoka shilingi 1,725,241 mwaka 2012 hadi kufikia shilingi 3,458,329 mwaka 2022.

Mkoa wa Ruvuma ni wa tisa katika kuchangia kwenye pato la Taifa kati ya mikoa 26 ya Tanzania bara.



Wakati huo huo uzalishaji wa madini ya makaa ya mawe katika Mkoa wa Ruvuma umekuwa chanzo kikubwa cha mapato ya serikali ambapo katika mwaka wa fedha wa 2023/2024,serikali imeweza kuuza tani 1,356,249.84 za makaa ya mawe zenye thamani ya Dola za Marekani Zaidi ya milioni 144.9.

Kwa mujibu wa taarifa ya Afisa Madini Mkazi Mkoa wa Ruvuma,kiasi hicho cha madini kimeuzwa katika kipindi cha kuanzia Julai hadi Septemba 2023 pekee.

Kupitia mauzo hayo serikali imekusanya kiwango cha mrabaha wa Dola za Marekani 3,937,434.98 na ada ya ukaguzi Dola za Marekani 914,034.68 na kwamba madini hayo yameuzwa ndani ya nchi,nchi Jirani,barani Ulaya na Asia kupitia bandari ya Mtwara na Dar es salaam.

Hata hivyo Ofisi ya Afisa Madini Mkazi Mkoa wa Ruvuma katika kipindi cha mwaka wa fedha 2023/2024 ilipangiwa kukusanya jumla ya shilingi bilioni 41 na kwamba katika kipindi cha kuanzia Julai hadi Desemba ofisi hiyo ilikusanya Zaidi ya shilingi bilioni 13 sawa na asilimia 64.

Uchimbaji na uuzaji wa makaa ya mawe mkoani Ruvuma ulianza mwaka 2011 kukiwa na Kampuni moja ya uchimbaji ya Tancoal Energy ambapo hadi kufikia mwka 2019 wadau wengi walijitokeza na kufanya uwekezaji mkubwa katika uzalishaji wa madini ya makaa ya mawe.

Kwa mujibu wa taarifa ya Afisa Madini Mkazi,kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita,Mkoa wa Ruvuma umeweza kupata wawekezaji wengi katika uchimbaji,ununuzi na uchenjuaji madini ya makaa ya mawe.

Ameutaja mchango wa sekta ya madini mkoani Ruvuma kuwa ni Pamoja kutoa ajira kwa mtu mmoja mmoja na kupunguza utegemezi,kuongeza fedha za kigeni kutokana na mauzo ya madini nje ya nchi na kuongeza mapato ya Halmashauri yatokanayo na ushuru wa huduma.

Hata hivyo taarifa hiyo imezitaja changamoto za sekta ya madini mkoani Ruvuma kuwa ni Pamoja na uharibifu wa mazingira kutokana na kukata miti na kuchafua vyanzo vya maji,ubovu wa barabara ya kutoka migodini na changamoto ya upimaji wa viwango vya ubora wa madini ya makaa ya mawe.

Changamoto nyingine ni kukosekana kwa teknolojia ya kisasa ya kuongeza ubora wa makaa ya mawe ili kushindana na soko,uwepo wa leseni za utafiti na uchimbaji ambazo haziendelezwi,uelewa mdogo wa taarifa za kijiolojia,utambuzi wa aina za madini,thamani yake na masoko ya madini jambo linalosababisha kusimama kwa uzalishaji wa madini ya shaba katika eneo la Mbesa wilayani Tunduru.

Ameitaja Mikakati ya kukabiliana na changamoto hizo kuwa ni kuendelea kuhamasisha wachimbaji wa makaa ya mawe na wawekezaji wengine kuleta mitambo ya kuosha madini ili kuongeza ubora,kusimamia kurudishwa kwa shughuli mgodi wa Tancoal Energy na kuendelea kutoa elimuya sheria ya madini.

## WANAWAKE RUVUMA WAPEWA MKOPO WA BILIONI TATU



SERIKALI imetoa zaidi ya shilingi bilioni tatu kukopesha vikundi 557 vya wanawake,vijana na wenye ulemavu mkoani Ruvuma.

Hayo yalisemwa na aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Kanali Laban Thomas wakati anazungumza kwenye kilele cha maadhimisho ya siku ya wanawake Duniani ambazo kimkoa zimefanyika wilayani Mbinga.

Amesema serikali imetoa fedha hizo katika kipindi cha kuanzia mwaka 2021 hadi 2023 ambapo mkopo huo umetokana na asilimia 10 ya mapato ya ndani ya Halmashauri mkoani Ruvuma

“Natoa wito kwa wanawake kujiunga kwenye vikundi vyenye tija na kuanzisha shughuli za ujasiriamali ambazo zitawainua kiuchumi na kuweza kurejesha mikopo mtakayokopa “,alisema.

Ameziagiza Halmashauri zote mkoani Ruvuma kuhakikisha zinatenga asilimia kumi ya mapato ya ndani na kukopesha vikundi vya wanawake,vijana na watu wenye ulemavu kila robo mwaka kama miongozo inavyoelekeza.

Akizungumzia changamoto zinazowakabili wanawake,Mkuu wa Mkoa amesema zipo changamoto zinazosababisha kuendelea kuwepo mfumo dume unaolindwa na mila na desturi potofu katika jamii.

Amewaasa wanawake kuendelea kutoa taarifa za unyanyasaji na ukatili zinapotokea pamoja na kuongeza ufahamu juu ya utambuzi wa haki na usawa kwa wote.

Risala ya wanawake wa Mkoa wa Ruvuma iliyosomwa na Joan Ngaponda kwenye maadhimisho hayo imesema maadhimisho hayo amesema mkoa una changamoto ya watoto kupata mimba za utotoni ambapo katika kipindi cha kuanzia Januari hadi Desemba 2023 matukio ya mimba za utotoni yalikuwa 2,068.

Risala imetaja moja ya visababishi vya kuendelea kuwepo umasikini katika ngazi ya kaya ni wanawake kuendelea kunyimwa haki hasa umiliki wa rasikimali ardhi.

Risala hiyo imebainisha kuwa katika cha kuanzia Januari hadi Desemba 2023 mashauri 2,859 ya ukatili yalitolewa taarifa na kushughulikiwa.

Hata hivyo risala ya wanawake imeipongeza serikali kwa kusimama kidete katika kulinda haki na kujenga usawa kwa jamii tote.

Kaulimbiu ya siku ya wanawake Duniani mwaka huu ni wekeza kwa wanawake kuharakisha maendeleo ya Taifa na ustawi wa jamii.

## BILIONI 2.24 KUTEKELEZA MIRADI YA MAJI SONGEA




Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais Dkt.Samia Suluhu Hassan imetenga Zaidi ya shilingi bilioni 2.238 kutekeleza miradi mitano ya maji katika Halmashauri ya Manispaa ya Songea mkoani Ruvuma katika mwaka wa fedha wa 2022/2023.

Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Songea (SOUWASA) Mhandisi Patrick Kibasa amesema hadi sasa fedha ambazo zimeidhinishwa kutekeleza miradi hiyo ni Zaidi ya shilingi bilioni 1.37.

Amesema kati ya fedha hizo,serikali imetoa Zaidi ya shilingi bilioni 145 kutekeleza mradi wa maji wa kimkakati wa miji 28 katika mji wa Songea na kwamba mradi huo umeanza kutekelezwa tangu Januari 2024.

Ameitaja miradi mingine inayotekelezwa katika Manispaa ya Songea kuwa ni ujenzi wa mradi wa maji katika kata ya Subira ambao umeidhinishiwa Zaidi ya shilingi bilioni 1.17 na kwamba mradi umetekelezwa kwa Zaidi ya asilimia 40.

Kwa mujibu wa Mkurugenzi huyo wa SOUWASA,serikali imeidhinisha Zaidi ya shilingi milioni 322 kutekeleza mradi wa maboresho ya uzalishaji maji katika mji wa Mbinga ambapo mradi umetelezwa kwa asilimia 100.

Ameitaja miradi mingine ambayo imekamilika kwa asilimia 100 ni mradi wa upanuzi wa mtandao wa maji safi katika mji wa Tunduru ambapo serikali imeidhinisha Zaidi ya shilingi milioni 355 na mradi wa maji eneo la viwanda kata ya Lilambo Manispaa ya Songea ambapo serikali imeidhinisha Zaidi ya shilingi milioni 415.

“Katika Manispaa ya Songea hadi kufikia mwaka 2023,wakazi 260,733 wanapata huduma ya maji sawa na asilimia 88.0,mahitaji ya Maji katika Manispaa ya Songea ni wastani lita milioni 20.593 kwa siku’’,alisisitiza Mhandisi Kibasa.

Hata hivyo amesema mwaka 2023 katika maeneo ya Manispaa ya Songea,uzalishaji wa maji ghafi ni wastani wa mita za ujazo 9,170 kwa siku na kwamba jumla ya maunganisho ya maji safi ni 22,465 ambapo upatikanaji wa huduma ya maji safi ni saa 23.15 kwa siku.

Mary Luoga na Joseph Komba ni wakazi wa Kata ya Lilambo Manispaa ya Songea ,wanamshukuru Rais Dkt.Samia Suluhu Hassan kwa kuidhinisha fedha kwa ajili ya kutekeleza mradi wa maji katika kata hiyo ambapo wananchi wananufaika kwa kupata maji safi na salama.

Diwani wa Kata ya Subira Manispaa ya Songea Mheshimiwa John Ngonyani kwa niaba ya wananchi wa Kata hiyo amesema tangu uhuru kata hiyo haijawahi kupata maji safi na salama ya bomba ambapo serikali ya awamu ya Sita imetoa fedha za kutekeleza mradi wa maji ambao unakwenda kupunguza kero ya maji.

Manispaa ya Songea ina wakazi wapatao 286,285 kwa mujibu wa takwimu za sensa ya watu na makazi ya mwaka 2022.

## TANROADS RUVUMA INAVYOJIVUNIA MIAKA MITATU YA RAIS SAMIA



***Mradi wa daraja la Ruhuhu katika Mto Ruhuhu unaomwaga maji yake ziwa Nyasa***

WAKALA wa barabara (TANROADS) mkoa wa Ruvuma,katika kipindi cha miaka mitatu imefanikiwa kutekeleza na kukamilisha miradi mbalimbali ya barabara ikiwemo ujenzi wa barabara ya Mbinga-Mbambabay yenye urefu wa kilomita 66 kwa kiwango cha lami iliyogharimu Sh.bilioni 129.361.

Aidha,TANROADS imekamilisha ujenzi wa daraja kubwa la Ruhuhu lenye urefu wa mita 98.01 linalounganisha wilaya ya Nyasa mkoani Ruvuma na wilaya ya Ludewa mkoa wa Njombe ambalo limekamilika na linatumika kwa shughuli za usafiri na usafirishaji.

Hayo yamesemwa  na Meneja wa TANROADS Mkoani Ruvuma Mhandisi Saleh Juma,wakati akitoa taarifa ya mafanikio katika kipindi cha miaka mitatu ya uongozi wa Rais Dkt Samia Suluhu Hassan.

Amesema,daraja hilo limejengwa kwa awamu mbili ambapo awamu ya kwanza ilihusisha ujenzi wa nguzo za daraja na ulitekelezwa na mkandarasi Lukolo Co Ltd na mhandisi mshauri wa mradi ni kampuni ya Crown Tech-Consult.

Saleh anabainisha kuwa,awamu ya pili imehusisha ununuzi na ufungaji wa kitanda cha daraja na kazi iliyofanywa na wataalam wa ndani kutoka(TANROADS) kwa kushirikiana na kampuni ya Jembela Ltd kwa gharama ya Sh.bilioni 8.976.

Anabainisha Zaidi kuwa ,wanaendelea na ujenzi wa barabara kutoka Amani Makolo-Ruanda ambayo sehemu ya mwendelezo wa ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Kitai-Lituhi-Ndumbi kwa kujenga kilomita 35 kwa kiwango cha lami.

Hata hivyo amesema,mradi huo ulianza mwezi Juni 2022 na ulitakiwa kukamilika mwezi Machi 2024,hata hivyo mkandarasi ameomba kuongezewa muda wa kukamilisha kazi ambapo mhandisi mshauri anapitia maombi hayo ili kujiridhisha na kutoa ushauri kwa wakala.

Ameutaja,mradi huo unatekelezwa na kampuni ya China Railway Seventh Group(CRSG) kwa gharama ya Sh.bilioni 60.481 na ujenzi wake umefikia asilimia 25.

Akizungumzia ujenzi barabara ya Ruanda-Lituhi-Ndumbi kwa kiwango cha lami Saleh amesema,ujenzi wa sehemu hiyo ni mwendelezo wa ujenzi wa wa barabara ya Kitai-Lituhi-Ndumbi ambayo itaanzia katika kijiji cha Ruanda hadi bandari ya Ndumbi urefu wa kilomita 50.

Amesema kazi ya usanifu imekamilika na zabuni ya mradi huo ilitangazwa tangu tarehe 31 Oktoba mwaka 2022 na serikali imeshatoa kibali cha utekelezaji na TANROADS ipo katika hatua za mwisho za maandalizi ya kutia saini mkataba wa ujenzi wa mradi huo

kwa mujibu wa Mhandisi Saleh,uthamini kwa ajili ya fidia wa mali zitakazo athirika na mradi umekamilika ambapo Sh.bilioni 2.9 zitatumika kulipa.

Amesema hivi sasa ofisi ya TANROADS ipo hatua za uwekwaji wazi taarifa hizo kwa waathirika kabla ya kuwasilishwa kwa mthamini mkuu wa serikali ili itiwe saini kwa ajili ya malipo.

Katika hatua nyingine Saleh amesema,serikali inatarajia kuanza ujenzi wa barabara ya Likuyufusi-Mkenda yenye urefu wa kilomita 124 kuelekea mpaka wa Tanzania na Msumbiji ambayo inatumika kusafirisha mazao na wananchi wa vijiji vya Mkenda,Mkayukayu,Mpitimbi na Likuyufusi.

Amesema,ujenzi wa barabara hiyo utafanyika kwa awamu ambapo awamu ya awamu ya kwanza itajengwa kilomita 62 kutoka Likuyu fusi hadi Mkayukayu na awamu ya pili itatoka Mkayukayu hadi Mkenda umbali wa kilomita 60.

## MRADI WA MAJI NGUMBO KUMALIZA CHANGAMOTO YA MAJI KATA ZA NGUMBO NA LIWUNDI




*Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira ikiongozwa na Mwenyekiti wake Mheshimiwa Jackson Kiswaga imetembelea na ,kukagua mradi wa maji Ngumbo wilayani Nyasa ambao unatekelezwa kwa gharama ya shilingi biliioni 2.5.*



*Kamati ya Bunge ya Maji na Mazingira ilipokagua mradi wa maji Kijiji cha Malungu Kata ya Tingi wilayani Nyasa uliogharimu Zaidi ya shilingi bilioni moj*

**SERIKALI YATOA BILIONI 66 KUTEKELEZA MIRADI YA MAJI 36 RUVUMA**



***Kushoto ni Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira Mheshimiwa Jackson Kiswaga***

KAMATI ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira,imekagua mradi wa maji Ngumbo Group uliopo kijiji cha Mbuli kata ya Ngumbo wilaya ya Nyasa mkaoni Ruvuma unaotekelezwa na wakala wa maji na usafi wa mazingira vijijini(RUWASA) na kuridhishwa na utekelezaji wa mradi huo.

Mwenyekiti wa kamati hiyo Jackson Kiswaga,ameipongeza serikali kupitia RUWASA kwa kuendelea kutekeleza miradi ya maji inayolenga kutatua changamoto ya upatikanaji wa huduma ya maji kwa wananchi hasa wanaoishi maeneo ya vijijini.

Amsema,serikali inafanya kazi nzuri kumaliza kero ya maji ili kuwaondolea wananchi usumbufu wa kutembea umbali mrefu kutafuta huduma hiyo ambapo katika mkoa wa Ruvuma serikali kupitia Ruwasa inatekeleza jumla ya miradi 36 yenye thamani ya Sh.bilioni 66.

Kiswaga amewaeleza wananchi wa kata ya Ngumbo kwamba,lengo la serikali ni kumaliza ujenzi wa mradi huo haraka ili wananchi wapata huduma ya maji na kamati yake itafuatilia fedha zilizobaki ili mkandarasi aweze kukamilisha ujenzi wa mradi huo haraka iwezekanavyo.

Aidha,amewataka wananchi kuhakikisha wanalinda vyanzo vya maji na kutunza mazingira ili miradi inayotekelezwa iweze kudumu kwa muda mrefu na kuleta tija.

“serikali inatumia fedha nyingi kutekeleza miradi hiyo kwa lengo la kusogeza huduma ya maji,hivyo ni wajibu wa kila mmoja kuhakikisha anatunza vyanzo vya maji na kuepuka kukata miti ovyo katika maeneo yao”alisema Kiswaga.

Mjumbe wa Kamati hiyo Charles Mwijage,amewataka wanaume wa kata ya Ngumbo ambao ni sehemu ya wanufaika wa mradi huo kujiandaa kuvuta maji kwenye nyumba zao ili kuunga mkono kauli ya Rais Dkt Samia Suluhu Hassan ya kumtua mama ndoo kichwani.

Aliyekuwa Naibu Waziri wa Maji Mheshimiwa Maryprisca Mahundi amesema,utekelezaji wa mradi huo unaendelea wakati wananchi tayari wameanza kunufaika kupata huduma ya maji kwa baadhi ya maeneo.

Amesema,serikali ya awamu ya sita chini ya Rais Dkt Samia Suluhu Hassan inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kuongeza mtandao wa maji kwenye vijiji ambavyo havijafikiwa na maji ya bomba ambapo amehaidi vijiji vilivyobaki vitapata maji mwishoni mwa mwezi April mwaka huu.

Naibu Waziri Mahundi,amemuagiza Meneja wa RUWASA wilaya ya Nyasa Mhandisi Masoud Samila kumsimamia Mkandarasi kampuni ya Nipo Africa Engineering Co Ltd inayejenga mradi huo ili afikishe mtandao wa maji kwenye maeneo yote yaliyopangwa kufikishwa huduma hiyo.

Mbunge wa Jimbo la Nyasa Mhandisi Stella Manyanya,amemshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kupeleka fedha kwa ajili ya miradi mbalimbali ya maendeleo ikiwemo miradi ya maji katika jimbo la Nyasa.

Meneja wa RUWASA wilaya ya Nyasa Mhandisi Masoud Samila amesema, mradi wa maji Ngumbo Group awamu ya 11 ulianza kutekelezwa mwezi Novemba 2023 na unatarajia kukamilika mwezi April 2024 na gharama za mradi huo ni Sh.bilioni 2,030,668,500.00.

Amesema,fedha hizo zinatoka mfuko wa maji wa Taifa,fedha za serikali kuu na fedha za mpango wa lipa kwa matokeo(P4R) na muda wa utekelezaji wa mradi ni siku 180.

Amezitaja faida za mradi huo utakapokamilika ni pamoja na wananchi wa vijiji vitano vya kata ya Ngumbo na Liwundi kupata huduma ya maji safi na salama kwenye maeneo yao.

## WANANCHI RUVUMA WAMSHUKURU RAIS KWA BANDARI YA NDUMBI



***Sehemu ya miundombinu katika bandari ya Ndumbi ziwa Nyasa***

WANANCHI wa Wilaya ya Nyasa mkoani Ruvuma wamemshukuru Rais Dkt.Samia Suluhu Hassan kwa kutenga fedha kiasi cha shilingi bilioni 12.2 kwa ajili ya ujenzi wa bandari mpya ya Ndumbi ziwa Nyasa.

Mbunge wa Jimbo la Nyasa Mhandisi Stella Manyanya akizungumza mjini Mbambabay amesema ujenzi wa bandari hiyo umekamilika kwa asilimia 100 na kwamba serikali pia imetenga shilingi bilioni 70 kwa ajili ya ujenzi wa bandari ya kisasa ya Mbambabay wilayani Nyasa.

“Kwa namna ya pekee tunamshukuru Jemedari wetu Rais Dkt.Samia Suluhu Hassan kwa kutoa mabilioni ya fedha kutekeleza miradi mikubwa ya bandari katika wilaya ya Nyasa’’,alisisitiza.

Manyanya amesema serikali inaendelea kuifungua wilaya ya Nyasa katika sekta ya usafiri na usafirishaji hivyo kutoa fursa kwa wawekezaji kufika kuwekeza katika wilaya hiyo yenye fursa nyingi za kiuchumi na uwekezaji,

Meneja wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari za Ziwa Nyasa Manga Gassaya akizungumzia utekelezaji wa ujenzi wa bandari ya Ndumbi,ameitaja miundombinu iliyojengwa katika bandari ya Ndumbi kuwa ni ujenzi wa Gati lenye

urefu wa mita 160 kwenda ziwani na sehemu ya kupokea lango la meli yenye urefu wa mita 40.

Miundombinu mingine iliyojengwa katika bandari ya Ndumbi ameitaja kuwa ni ghala la kuhifadhia mizigo lenye mita za ukubwa 1,020,eneo la sakafu ngumu kwa ajili ya kuhifadhia mizigo isiyoathiriwa na mvua lenye mita za ukubwa 9030 na jengo la kupumzikia abiria lenye uwezo wa kuhudumia abiria 70,000 kwa mwaka.

Gassaya amesema bandari ya Ndumbi baada ya kukamilika Desemba 2022 imeongeza uwezo wa kuhudumia shehena kwa bandari za ziwa Nyasa kwa mwaka kutoka tani 76,000 hadi kufikia tani 110,000.

Amesema bandari hiyo pia imeongeza uwezo wa kuhudumia abiria kutoka abiria 56,000 kwa mwaka hadi kufikia abiria 126,000.

Meneja huyo wa bandari za ziwa Nyasa amesema serikali pia imeanza kutekeleza ujenzi wa bandari mpya ya kisasa ya Mbambabay lengo likiwa ni kuimarisha ushoroba wa maendeleo ya Mtwara ambayo ni njia fupi na rahisi kuhudumia mizigo ya Malawi kutokea bandari ya Mtwara.

“Serikali ya Awamu ya Sita imetenga shilingi bilioni 70 kuanza kutekeleza mradi huo ambao unatarajia kukamilika ndani ya miezi 24,ujenzi wa bandari ya Mbambabay ukikamilika utaongeza uwezo wa kuhudumia shehena ya mizigo katika bandari kutoka tani 110,000 hadi kufikia tani 550,000 kwa mwaka’’,alisema.

Hata hivyo amesema baada ya ujenzi wa bandari mpya ya Mbambabay kukamilika,makao makuu ya bandari za ziwa Nyasa yatahamia Mbambabay wilayani Nyasa mkoani Ruvuma kutoka bandari ya Kiwira iliyopo wilayani Kyela mkoani Mbeya.

Amesema kutokana na maboresho makubwa yaliyofanywa na serikali katika bandari za ziwa Nyasa,katika kipindi cha miezi sita ya mwaka 2023/2024 bandari zimehudumia jumla ya abiria 7,358 na mizigo tani 1,828.6.

Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA) inasimamia bandari 15 katika ziwa Nyasa zilizopo katika mikoa ya Ruvuma,Mbeya na Njombe.

## RAIS SAMIA ALIVYOLETA TABASAMU KWA WANAFUNZI WA KIKE RUVUMA



SERIKALI ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais Dkt.Samia Suluhu Hassan imetoa zaidi ya shilingi bilioni 15 kupitia program ya Uboreshaji Elimu ya Sekondari (SEQUIP) kujenga sekondari mpya za mfano 21 mkoani Ruvuma.

Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Kanali Ahmed Abbas Ahmed anasema kati ya sekondari hizo,katika awamu ya kwanza ya SEQUIP zimejengwa sekondari 11 zilizogharamu shilingi bilioni 7.7 ikiwemo sekondari moja ya wasichana ya Kitaifa iliyojengwa wilayani Namtumbo kwa gharama ya shilingi bilioni nne.

Kulingana na Mkuu wa Mkoa katika awamu ya pili ya SEUIP serikali imetoa zaidi ya shilingi bilioni 6.44 kujenga sekondari mpya za sekondari 10 katika Halmashauri zote nane za Mkoa wa Ruvuma.

Anasisitiza kuwa Rais Dkt.Samia Suluhu Hassan ametoa fedha hizo ili kujenga shule mpya za sekondari za kata katika kata zisizo na shule na kata zenye wanafunzi wengi zaidi ukilinganisha na miundombinu ya shule zilizopo.

Afisa Elimu wa Mkoa wa Ruvuma Mwl.Edith Mpinzile anasema katika Halmashauri ya Tunduru zimejengwa shule tano za sekondari kupitia mradi wa SEQUIP na kwamba katika Halmashauri ya Namtumbo zimejengwa shule za sekondari tatu ikiwemo shule ya kitaifa ya wasichana ya Mkoa wa Ruvuma.

Kulingana na Afisa Elimu huyo katika Halmashauri ya Manispaa ya Songea zimejengwa sekondari mbili,Halmashauri ya Madaba sekondari mbili, Halmashauri ya Songea sekondari mbili, Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga sekondari mbili,Halmashauri ya Mji wa Mbinga sekondari mbili na Halmashauri ya Nyasa sekondari mbili.

“Mradi wa SEQUIP umewezesha kila shule ya sekondari kuwa na jengo la utawala,vyumba vya madarasa nane, vyoo matundu 12,mfumo wa maji, maabara tatu,maktaba tatu,kichomea taka na jengo la TEHAMA ”,anasema.

Anasema sekondari 20 zilizojengwa mkoani Ruvuma kupitia SEQUIP awamu ya kwanza na ya pili zimekamilika na kuanza kuchukua wanafunzi ambapo sekondari moja inaendelea kujengwa katika Kata ya Tanga Manispaa ya Songea.

Wanafunzi walioanza masomo katika sekondari hizo wanaipongeza serikali kwa kuwajengea sekondari hizo ambazo zimemaliza changamoto ya wanafunzi kusafiri umbali mrefu kufuata sekondari.

Juma Issa na Khadija Kassim ni wanafunzi wa sekondari mpya Kata ya Tinginya wilayani Tunduru wanasema kabla ya ujenzi wa sekondari hii,wanafunzi waliofaulu katika Kata hiyo walikuwa wanakwenda kusoma katika sekondari ya Nakapanya ambayo ipo umbali wa kilometa 40.

“Kutokana na umbali huo wanafunzi wengi waliacha shule,utoro ulikuwa mwingi na Watoto wa kike walipata mimba baada ya kukumbwa na vishawishi vingi’’,alisema Khadija Kassim.

Mariam Ismail ni Mwananchi kutoka Kijiji cha Tinginya wanasema kabla ya sekondari hiyo wazazi walipata gharama kubwa kwa Watoto wao ikiwemo nauli ya kusafiri Kwenda sekondari ya Nakapanya ambapo baadhi ya wazazi walishindwa kumudu ambapo hivi sasa wanamshukuru Rais kwa kuwajengea sekondari hiyo.

Mkuu wa sekondari ya Tinginya Romatus Ndoa anasema walipokea kiasi cha shilingi milioni 560 ambazo zimetumika kujenga jengo la utawala,madarasa manane,vyumba vitatu vya maabara,jengo la TEHAMA,kichomea taka,minara miwili ya maji na vyoo matundu 12,

Anabainisha kuwa wanafunzi wameanza masomo tangu Januari mwaka huu ambapo sekondari hiyo ya kisasa na mazingira ya kuvutia imeondoa kabisa changamoto ya wanafunzi wa Kata ya Tinginya kusafiri umbali mrefu.

Teresia Ng’ombo ni Kaimu Mkuu wa shule ya sekondari Tuwemacho wilayani Tunduru ambaye anasema wamepokea wanafunzi 70 kati ya 87 waliopangiwa kuanza kidato cha kwanza katika sekondari hiyo.

Zamda Yusufu na Siyawezi Libadi ni wanafunzi wa kidato cha kwanza katika sekondari ya Tuwemacho wanasema ujenzi wa sekondari hiyo umemaliza tatizo la wanafunzi kusafiri kilometa 45 hadi sekondari ya Namasakata kufuata shule.

Kwa upande wake Kaimu Mkuu wa shule ya sekondari Mputa wilayani Namtumbo Filbert Mbunda anasema sekondari hiyo imepokea wanafunzi wa kidato cha kwanza wapatao 157 kati yao waliomaliza darasa la saba mwaka 2023 ni 135 na waliomaliza darasa la saba mwaka 2022 ni 22.

Anasema kabla ya kuanza sekondari hiyo wanafunzi wote waliokuwa wanafaulu darasa la saba walipelekwa sekondari ya Mbunga iliyopo Kata ya Kitanda ambapo walikuwa wanatembea umbali wa kilometa 30 kila siku hali iliyosababisha wanafunzi wengi kuacha shule.

Naye Mkuu wa shule ya sekondari ya Lilondo Subira Mapunda anasema baada ya shule hiyo kukamilika wamepokea wanafunzi wa kidato cha kwanza ambao walikuwa wanasafiri umbali wa kilometa 20 hadi sekondari ya Wino ambapo hivi sasa wanafunzi wanafurahia mazingira mazuri ya kujifunzia.

Ado Kawonga ni Kaimu Mkuu wa sekondari ya Mtopesi iliyojengwa katika Kijiji cha Lugagara Halmashauri ya Wilaya ya Songea anasema mara baada ya kukamilisha ujenzi wamepokea wanafunzi 71 wa kidato cha kwanza hivyo kumaliza changamoto ya wanafunzi kutembea kilometa 30 kila siku kufuata sekondari ya Kilagano.

Petro Liweli ni Mkuu wa shule ya sekondari ya Dkt.Lawrence Gama iliyopo Kata ya Mkuzo Manispaa ya Songea anasema wamepokea jumla ya wanafunzi wa kidato cha kwanza 200 ambao wameanza masomo mwaka huu .

Serikali kupitia SEQUIP awamu ya pili katika mwaka 2022/2023 imetoa zaidi ya shilingi bilioni 100 kwa ajili ya ujenzi wa sekondari mpya za kata 176 kati ya hizo sekondari kumi zimejengwa mkoani Ruvuma.

Serikali ya Awamu ya Sita imtenga shilingi Trilioni 1.2 kupitia program ya SEQUIP kujenga shule mpya za sekondari 1000 katika nchi nzima zikiwemo sekondari mpya 26 za kitaifa kwa ajili ya wasichana ambazo zinajengwa kwa kipindi cha miaka mitano katika nchi nzima

## SEKONDARI YA WASICHANA YA DKT SAMIA FAHARI YA RUVUMA



Muonekano kutoka juu wa shule ya sekondari ya wasichana ya Dkt Samia Suluhu Hassan iliyojengwa wilayani Namtumbo mkoani Ruvuma kupitia Program ya Uboresha Elimu ya Sekondari (SEQUIP) ambapo serikali imetoa shilingi bilioni nne kutekeleza mradi huo.

Sekondari hiyo yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi zaidi ya 1000 imeanza kuchukua wanafunzi wa kidato kwa kwanza na cha tano




Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais Dkt Samia Suluhu Hassan imetenga zaidi ya shilingi bilioni nne kutekeleza mradi wa ujenzi wa sekondari ya mfano ya wasichana mkoani Ruvuma yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi wa kidato cha kwanza hadi cha sita.

Sekondari hiyo iliyojengwa wilayani Namtumbo kupitia Program ya Uboreshaji Elimu ya Sekondari (SEQUIP) tayari imeanza kuchukua wanafunzi wa kidato cha kwanza na cha tano

**MIAKA MITATU YA RAIS SAMIA,MRADI WA UJENZI WA BANDARI YA KISASA MBAMBABAY WAANZA**



Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan imeanza kutekeleza ujenzi wa bandari mpya ya kisasa ya Mbambabay ziwa Nyasa wilayani Nyasa mkoani Ruvuma kwa gharama ya shilingi bilioni 70 lengo likiwa ni kuimarisha ushoroba wa maendeleo ya Mtwara ambayo ni njia fupi na rahisi kuhudumia mizigo ya Malawi kutokea bandari ya Mtwara.

Mradi huo unatarajia kukamilika ndani ya miezi 24,ujenzi wa bandari ya Mbambabay ukikamilika utaongeza uwezo wa kuhudumia shehena ya mizigo katika bandari kutoka tani 110,000 hadi kufikia tani 550,000 kwa mwaka na kwamba baada ya ujenzi wa bandari mpya ya Mbambabay kukamilika,makao makuu ya bandari za ziwa Nyasa yatahamia Mbambabay wilayani Nyasa mkoani Ruvuma kutoka bandari ya Kiwira iliyopo wilayani Kyela mkoani Mbeya.

Kutokana na maboresho makubwa yaliyofanywa na serikali katika bandari za ziwa Nyasa,katika kipindi cha miezi sita ya mwaka 2023/2024 bandari zimehudumia jumla ya abiria 7,358 na mizigo tani 1,828.6.Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA) inasimamia bandari 15 katika ziwa Nyasa zilizopo katika mikoa ya Ruvuma,Mbeya na Njombe.



## KERO YA MAJI SONGEA KUBAKIA HISTORIA



SERIKALI imeanza kutekeleza ujenzi wa mradi wa maji wa miji 28 katika mji wa Songea mkoani Ruvuma unaogharimu shilingi bilioni 145.7.

Kukamilika kwa mradi huu kutaleta manufaa makubwa ikiwemo SOUWASA kuongeza uwezo wa kuzalisha maji kutoka lita milioni 11.58 kwa siku hadi kufikia lita milioni 42.581 kwa siku,

Mradi huo unakwenda kumaliza kero ya maji katika Manispaa ya Songea kwa sababu upatikanaji wa maji utakuwa na uwezo wa kuwahudumia wananchi wapatao 440,794.

# RUVUMA KUPANDA MITI KIBIASHARA HEKTA LAKI MOJA



MKOA wa Ruvuma unatarajia kupanda hekari laki moja za miti kibiashara kwa kipindi cha miaka kumi kuanzia mwaka 2015 hadi 2025.

Afisa Maliasili Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Afrikanus Challe amesema upandaji miti huo unatekelezwa katika maeneo ya serikali kuu,serikali za mitaa,vyuo na shule na kwamba Mkoa umekuwa mstari wa mbele katika kuhamasisha upandaji miti na utunzaji mazingira.

“Uhamasishaji huu unakwenda sanjari na utekelezaji wa kampeni ya kitaifa ya upandaji miti inayoongozwa na Rais Dkt.Samia Suluhu Hassan ambao unafanyika katika Halmashauri zote’’,alisisitiza.

Amesema katika msimu wa mwaka 2023/2024 Mkoa wa Ruvuma unatarajia kupanda miche ya miti Zaidi ya milioni nne na kwamba miti hiyo ni kwa ajili ya mbao, vyanzo vya maji na matunda.

**BANDARI YA NDUMBI KUUNGANISHWA NA LAMI**




Serikali kupitia Wizara ya Ujenzi imetenga zaidi ya shilingi bilioni 150 kujenga barabara ya lami nzito kutoka Kijiji cha Ruanda Wilaya ya Mbinga hadi bandari ya Ndumbi Wilaya ya Nyasa mkoani Ruvuma.Serikali imetoa shilingi bilioni 12.2 kujenga bandari ya kimkakati ya Ndumbi.



## RAIS SAMIA ATOA MBOLEA YA RUZUKU TANI 93,000 RUVUMA



SERIKALI ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais Dkt.Samia Suluhu Hassan imetoa Zaidi ya tani 93,000 za mbolea ya ruzuku katika mkoa wa Ruvuma katika msimu wa mwaka 2023/2024.

Takwimu hizo zinaonesha kuwa kiasi hicho cha mbolea ya ruzuku kilichotolewa mkoani Ruvuma ni kikubwa ukilinganisha na mbolea ya ruzuku iliyotolewa katika mikoa mingine nchini.

Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Kanali Ahmed Abbas Ahmed amesema Rais Dkt.Samia Suluhu Hassan ametoa kipaumbele kikubwa cha mbolea ya ruzuku katika msimu huu mkoani Ruvuma ukilinganisha na usambazaji wa mbolea hiyo katika msimu uliopita.

Hata hivyo amesema serikali ya Awamu ya Sita imeendelea kufanya maboresho makubwa katika sekta ya kilimo kwa kuendelea kuboresha miundombinu ya kilimo ,mifumo ya ruzuku ya pembejeo na vyombo vya usafiri kwa maafisa ugani.

Amesema uboreshaji huo umesababisha kuongezeka kwa uzalishaji wa mazao kutoka tani 1,623,509.57 msimu wa mwaka 2020/2021 hadi kufikia tani 1,823,509.59 katika msimu wa mwaka 2022/2023.
“Serikali imetoa pikipiki 281 kwa maafisa ugani wote wa Kata na vijiji katika Mkoa mzima kwa lengo la kuwawezesha maafisa hao kuwafikia wakulima ili kutoa huduma za ugani kwa wakulima na mashine saba za kupima afya ya

udongo’’,alisema RC Abbas.

Hata hivyo amesema kutokana na kushuka kwa bei ya mbolea ya ruzuku kutoka mfuko mmoja kati ya shilingi 130,000 hadi shilingi 140,000 hadi kufikia kati ya 50,000 na 70,000 msimu huu, Wakulima wengi mkoani Ruvuma wamemudu gharama za mbolea, hali iliyosababisha wakulima kuongeza ukubwa wa mashamba na kutumia mbolea za viwandani kwa wingi.

Amesema Mkoa wa Ruvuma kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo wamejenga maghala 31 yenye uwezo wa kuhifadhi tani1,000 kila mmoja katika Halmashauri za Madaba ambako yamejengwa maghala 11,Halmashauri ya Songea maghala 12 na Namtumbo maghala nane.

Kanali Abbas amesema Mkoa wa Ruvum una utoshelevu wa chakula na kuwa na ziada na kwamba Chakula kilichozalishwa katika msimu 2022/2023 kinatarajia kutumika hadi msimu wa 2023/2024 ambapo mazao ya chakula zilizalishwa tani 1,598,163 na kati ya hizo zao la mahindi zimezalishwa jumla ya tani 1,043,324.
Kwa mujibu wa sensa ya watu ya 2022 Mkoa una jumla ya watu 1,848,794 ambao mahitaji yao ya chakula aina ya wanga ndani ya Mkoa kwa msimu 2023/2024 ni tani 554,638 na kuufanya Mkoa kuwa na ziada ya chakula tani 1,043525.



# RC RUVUMA ANAVYOIMARISHA MAHUSIANO NA NCHI JIRANI



Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Kanali Ahmed Abbas Ahmed anaendelea kutekeleza maagizo ya Rais Dkt Samia Suluhu Hassan ya kuimarisha mahusiano na nchi jirani ya Msumbiji ambapo ametembelea eneo la Kongreso Jimbo la Niassa nchini Msumbiji




Hapa ni eneo la Kongreso Jimbo la Niassa nchini Msumbiji ni eneo ambalo lipo mpakani na Tanzania kijiji cha Mkenda wilayani Songea,nchi hizi zinatengenishwa na Mto Ruvuma

## MSUMBIJI KUUNGANISHWA NA UWANJA WA NDEGE WA SONGEA



Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Kanali Ahmed Abbas Ahmed amesema utakapokamilika mradi wa ujenzi wa barabara ya lami nzito kutoka Likuyufusi hadi Mkenda mpakani mwa Tanzania na Msumbiji itakuwa ni fursa kwa wananchi wa Msumbiji kuutumia uwanja wa ndege Songea hivyo kuongeza uchumi wa Mkoa na Taifa.

Kanali Abbas amesema hayo wakati anazungumza katika Kituo cha Uhamiaji cha Mkenda wilayani Songea baada ya kukagua miundombinu ya barabara hiyo yenye urefu wa Zaidi ya kilometa 120.

Amemshukuru Rais Dkt.Samia Suluhu Hassan kwa kutenga Zaidi ya shilingi bilioni 74 kuanza kutekeleza awamu ya kwanza ya ujenzi wa barabara ya lami kilometa Zaidi ya 60 kuanzia Likuyufusi hadi njia panda ya Muhukuru wilayani Songea.

“Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kuamua kuunganisha Mkoa wa Ruvuma na nchi ya Msumbiji kwa kuanza kujenga barabara ya lami kilometa 60 ’’,alisema RC Abbas.

Mkuu wa Mkoa pia amemshukuru Rais Dkt Samia kwa kutoa fedha za upanuzi na ukarabati wa uwanja wa Ndege Songea ambapo serikali imetumia zaidi ya shilingi bilioni 37 kutekeleza mradi huo.

Hata hivyo amesema ujenzi barabara ya Likufusi - Mkenda mpakani na nchi ya Msumbiji,itakuwa fursa kwa wananchi wa nchi hiyo kutumia barabara hiyo hadi mjini Songea kisha kutumia uwanja wa ndege wa Songea kusafiri sehemu mbalimbali nchini.

Amesisitiza kuwa Rais Samia amewaagiza kuzitumia fursa zilizopo mkoani Ruvuma kwa kutoa fursa na kufungua shughuli za kiuchumi katika Mkoa wa Ruvuma bila kuathiri suala zima la ulinzi na usalama katika Mkoa ambao upo mpakani na nchi za Msumbiji na Malawi.

## TARURA RUVUMA YATENGEWA BILIONI 22.5 KWA AJILI YA MIUNDOMBINU



***Mwenye suti ya bluu ni Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma akikagua barabara ya Matomondo-JKT Mlale yenye urefu wa kilometa 21 inayosimamiwa na TARURA***

Serikali inayoongozwa na Rais Dkt.Samia Suluhu Hassan Kwa mwaka wa fedha 2023/2024 katika bajeti ya miundombinu ya barabara Mkoa wa Ruvuma umeidhinisha Zaidi ya shilingi bilioni 22.5.

Kaimu Meneja wa TARURA Mkoa wa Ruvuma Mhandisi Silivano Ngonyani amesema hadi kufikia Machi 2024,TARURA Ruvuma imepokea Zaidi ya shilingi bilioni 8.3 ambayo ni sawa na asilimia 37 ya bajeti ya matengenezo ya barabara.

Mhandisi Ngonyani amesema TARURA inaendelea kufanyia matengenezo barabara na madaraja yaliyobomoka kutokana na mvua za masika zinazoendelea ambapo katika Mkoa wa Ruvuma jumla ya madaraja 19 yameboka na kwamba ili kurejesha mawasiliano ya madaraja na maungio ya barabara zinahitajika Zaidi ya shilingi bilioni 2.2.

Hata hivyo amezitaja juhudi zinazofanywa na TARURA ili kukabiliana na changamoto ya kusombwa madaraja na maungio ni Pamoja na kuwaelekeza wananchi kutumia njia mbadala na kuomba bajeti ya dharura ili kurejesha miundombinu katika hali yake.

Ameyataja baadhi ya maeneo yanahitaji ujenzi wa madaraja mapya ili kuweza kuhimili wingi wa maji unaosababishwa na mabadiliko ya tabianchi.

Miongoni mwa madaraja mapya yaliyojengwa na TARURA ni daraja la Mto Njoka lililopo katika Kata ya Kizuka Halmashauri ya Wilaya ya Songea ambapo serikali imetoa Zaidi ya shilingi milioni 600 kutekeleza mradi huo ambao umekamilika kwa asilimia 100.

Akizungumzia daraja hilo Mhandisi Ngonyani amesema kukamilika kwa daraja hilo ni muendelezo wa kazi zinazofanywa na serikali ya awamu ya sita ya kuendeleza uboreshaji wa barabara na madaraja na kwamba ujenzi wa madaraja unaendelea katika wilaya zote za Mkoa wa Ruvuma.

Wakati huo huo Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Kanali Ahmed Abbas Ahmed amekagua mradi wa ujenzi barabara ya Matomondo hadi JKT Mlale Halmashauri ya Wilaya ya Songea yenye urefu wa Kilometa 21 inayojengwa kwa kiwango cha lami nyepesi.

Kanal Abbas ameridhishwa na utekelezaji wa mradi huo ambao unatekelezwa kwa awamu ambapo hadi sasa serikali imetoa zaidi ya shilingi bilioni 5.9 kutekeleza mradi huo.

Barabara hii inaunganisha kata za Mbingamharule na Magagura ambazo zinawazalishaji wakubwa wa mazao ya chakula na biashara hivyo wananchi hao wataunganishwa na barabara Kuu ya Songea-Mbambabay

**JARIDA HILI LIMEANDALIWA NA SEKRETARIETI YA MKOA WA RUVUMA**

**Kupitia Kitengo cha Mawasiliano Serikalini Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma**

**S.L.P 74 SONGEA**

**57180 RUVUMA**
**SIMU Nambari.025- 2602256/2602238**
**FAX Na.2602144**
**E-MAIL:** ras.ruvuma@tamisemi.go.tz
**TOVUTI:www.ruvuma.go.tz**
**INSTAGRAM; rs ruvuma**
**FACEBOOK: rs ruvuma**

**WITTER:rs ruvuma**

**YOU TUBE; rs ruvuma**